**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**

**MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 08/02/2023 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA**

**Wajumbe waliohudhuria**:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pascal M. Kihanga | __ | Mstahiki Meya – Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Ally H.Machela | __ | Mkurugenzi wa Manispaa -Katibu |
| 3. | Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele | __ | Naibu Meya – Makamu Mwenyekiti |
| 4. | Mhe. Emmy Kiula Rajabu | __ | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ally Rashid Kalungwana | __ | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Joel Albert Kisome | __ | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Latifa Said Ganzel | __ | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Issa Kiduka | __ | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Abdallah Ally Meya | __ | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Hassan Madadi Maringo | __ | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Samuel Alfred Msuya | __ | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Mch. Thomas Benedict Butabile | __ | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Warda Omari Bazia | __ | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani | __ | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Salima Bonzo Mbandu | __ | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Peter Joel Dhahabu | __ | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Rahma Lashayo Maumba | __ | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Eng. Hamisi Hamadi Ndwata | __ | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Namala Johaness Mchunguzi | __ | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Madaraka S. Bindyanguze | __ | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Amini Abdallah Tunda | __ | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Aisha Ahmad Kitime | __ | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Zinduna Kombo Selemani | __ | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Amina Hussein Zihuye | __ | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Grace Luwis Mkumbae | __ | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu | __ | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Lt.Col(Mst) Ahmed S. Mazora | __ | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Zuberi George Mkalaboko | __ | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu | __ | Mjumbe |
| 30. | Mhe. Rashid Ramadhani Matessa | __ | Mjumbe |
| 31. | Mhe. Salum Mrisho Chunga | __ | Mjumbe |
| 32. | Mhe. Marco Mathias Kanga | __ | Mjumbe |
| 33. | Mhe. Athumani Omary Lujuo | __ | Mjumbe |
| 34. | Mhe. Hamisi Ally Kilongo | __ | Mjumbe |
| 35. | Mhe. Mwanaidi Ebrahim Ngulungu | __ | Mjumbe |
| 36. | Mhe. Melchior Peter Mwamnyanyi | __ | Mjumbe |

**Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb) | __ | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma ( Mb) | __ | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Norah Mzeru (Mb) | __ | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah | __ | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Selestini Savini Mbilinyi | __ | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Hadija Kombo Kibati | __ | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Seif Zahoro Chomoka | __ | Mjumbe |

**Viongozi waliohudhuria:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Rebeca Nsemwa | __ | Mkuu wa Wilaya ya Morogoro |
| 2. | Ndg. Ruth John | __ | Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro |
| 3. | Ndg. Leopold Ngirwa Huduma za Serikali za Mitaa | __ | Kny: Katibu Tawala Mkoa Msaidizi, |
| 4. | Mhe. Fikiri H. Juma | __ | Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Morogoro |
| 5. | Mhe. Aziza Omary | __ | Katibu Mkuu wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini |
| 6. | Mhe. Maulidi H. Chambilila | __ | Katibu Mwenezi na Siasa CCM Wilaya Morogoro Mjini |
| 7. | Eng. Bertam B. Minde | __ | Mhandisi kutoka MORUWASA |
| 8. | Ndg. James M. Hiza | __ | Meneja wa TANROADS Mkoa |
| 9. | Ndg. Boniphace Kapumbe | __ | Kutoka TARURA Wilaya |
| 10. | Ndg. Haji Mohamed | __ | Kaimu Afisa Usalma Wilaya ya Morogoro |
| 11. | Ndg. Martin Gwandu | __ | Afisa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro |
| 12. | Ndg. Fadhili Chilombe | __ | Meneja wa TANESCO Mkoa |

**Wakuu wa Divisheni na Vitengo waliohudhuria:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Pilly R. Kitwana | __ | Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Rasilimali Watu wa Manispaa - Katibu |
| 2. | Ndg. Jeremiah Lubeleje | __ | Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu wa Manispaa |
| 3. | Ndg. Christina Kayuki | __ | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu wa Manispaa |
| 4. | Dr. Tito Kagize | __ | Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Manispaa |
| 5. | Ndg. Dauson Jeremiah | __ | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Hifadhi ya Mazingira wa Manispaa |
| 6. | Ndg. Salum A. Papen | __ | Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria wa Manispaa |
| 7. | Ndg. Shaban Duru | __ | Afisa Rasilimali watu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | Ndg. Evance Y. Kutona | __ | Afisa Usafirishaji wa Manispaa |
| 9. | Ndg. Epiphania Matafu | __ | Afisa Kilimo |
| 10. | Ndg. Safia Kingwahi | __ | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa wa Manispaa |
| 11. | Ndg. Samwel Subi | __ | Mkuu wa Kitengo cha Usafishaji na Udhibiti wa Taka wa Manispaa |
| 12. | Ndg. Jafari A. Makupula | __ | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi na Ununuzi wa Manispaa |
| 13. | Ndg. Lusubilo Mwaisunga | __ | Katibu TSC wa Manispaa |
| 14. | Ndg. Festus Herman | __ | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji wa Manispaa |
| 15. | CPA. Andrew Masanja | __ | Mkaguzi wa Ndani wa Manispa. |
| 16. | Ndg. Faraja Maduhu | __ | Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii wa Manispaa |
| 17. | Dr. Charles R. Mkombachepa | __ | Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Manispaa |
| 18. | Ndg. Winfred A. Kipako | __ | Afisa Tarafa wa Manispaa |
| 19. | Ndg. Martin Mzuanda | __ | Kaimu Afisa Afya wa Manispaa |
| 20. | Ndg. Feliciana Katemana | __ | Mratibu wa TASAF wa Manispaa |
| 21. | Ndg. Upendo Elias | __ | Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa |
| 22. | Ndg. Chausiku Masegenya | __ | Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi wa Manispaa |
| 23. | Ndg. Adam T. Shayo | __ | Mthibiti Ubora wa Shule Wilaya |
| 24. | Eng. Juma Gwisu | __ | Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mijini wa Manispaa |
| 25. | Ndg. Emeline E. Kihunrwa | __ | Afisa Mipangomiji wa Manispaa |
| 26. | Ndg. Lilian Henerico | __ | Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Manispaa |
| 27. | Ndg. Zena Cornel Lutego | __ | Kaimu Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa |

**Watendaji wa Kata waliohudhuria:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Baraka Lemaha | __ | Mtendaji wa Kata ya Mindu |
| 2. | Ndg. Jenifer Stephen Rashid | __ | Mtendaji wa Kata ya Kauzeni |
| 3. | Ndg. Mariam Khalid Ngoda | __ | Mtendaji wa Kata ya Uwanja wa Taifa |
| 4. | Ndg. Laurent Masanja | __ | Mtendaji wa Kata ya Tungi |
| 5. | Ndg. Maria J. Shine | __ | Mtendaji wa Kata ya Kingo |
| 6. | Ndg. Asma M. Mpore | __ | Mtendaji wa Kata ya Mji Mkuu |
| 7. | Ndg. Andrew E. Luka | __ | Mtendaji wa Kata ya Mji Mpya |
| 8. | Ndg. Tatu H. Ally | __ | Mtendaji wa Kata ya Kihonda |
| 9. | Ndg. Bright Sospeter | __ | Mtendaji wa Kata ya Kilakala |
| 10. | Ndg. Said R. Maleta | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Luhungo |
| 11. | Ndg. Mariam S. Rajabu | __ | Mtendaji wa Kata ya Lukobe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Ndg. Sekela Konga | __ | Mtendaji wa Kata ya Mwembesongo |
| 13. | Ndg. Hendrica G. Lokilo | __ | Mtendaji wa Kata ya Mlimani |
| 14. | Ndg. Witness Matowo | __ | Mtendaji wa Kata ya Kihonda Magorofani |
| 15. | Ndg. Hamisi Ally Ismail | __ | Mtendaji wa Kata ya Mkundi |
| 16. | Ndg. Josepher B. Kisaka | __ | Mtendaji wa Kata ya Magadu |
| 17. | Ndg. Prisca Mawallah | __ | Mtendaji wa Kata ya Boma |
| 18. | Ndg. Helena W. Mgallah | __ | Mtendaji wa Kata ya Bigwa |
| 19. | Ndg. Amina Said Mhina | __ | Mtendaji wa Kata ya Mafiga |
| 20. | Ndg. Lilian P. Kagoma | __ | Mtendaji wa Kata ya Sultan Area |
| 21. | Ndg. Sekela A. Kajigili | __ | Mtendaji wa Kata ya Mazimbu |
| 22. | Ndg. Merina C. Singano | __ | Mtendaji wa Kata ya Kichangani |
| 23. | Ndg. Fatma H. Mkwenda | __ | Mtendaji wa Kata ya Sabasaba |
| 24. | Ndg. Sada Said Mpina | __ | Mtendaji wa Kata ya Mbuyuni |
| 25. | Ndg. Mwajabu R. Hassani | __ | Mtendaji wa Kata ya Mafisa |
| 26. | Ndg. Christina Ngonyani | __ | Mtendaji wa Kata ya Mzinga |
| 27. | Ndg. Pius Liberia Michael | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Chamwino |
| 28. | Adv. Masanja Nkinga | __ | Mtendaji wa Kata ya Luhungo |

**Sekretarieti:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Daudi A. Kibwana | __ | Katibu wa Mikutano |
| 2. | Ndg. Deogratias Butabile | __ | Katibu wa Mikutano |
| 3. | Ndg. Mwasi E. Mulwambo | __ | Katibu wa Mikutano |
| 4. | Ndg. Theresia Mbena | __ | Katibu wa Mikutano |
| 5. | Ndg. Jimmy Katabaruki | __ | Katibu wa Mikutano |
| 6. | Ndg. Lilian Lemunge | __ | Katibu wa Mikutano |

HMM/BM/44/ 2022/2023 Kufungua mkutano

Baada ya akidi ya Wajumbe kutimia, Katibu alimkaribisha Mstahiki Meya ili afungue mkutano.

Mstahiki Meya (Mwenyekiti) aliwaongoza Wajumbe na watu wote waliohudhuria mkutano kuimba wimbo wa Taifa na alisoma Dua ya kuiombea Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Baada ya Dua, Mstahiki Meya aliwakaribisha Wajumbe na alifungua mkutano saa 5:03 asubuhi. Aidha, alitoa taarifa ya udhuru wa Waheshimiwa Wabunge watatu na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani.

**Ukaribisho wa Mhe. Rebeca Nsemwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro**

Mstahiki Meya alimkaribisha Mhe. Rebeca Nsemwa – Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ili awasalimie Waheshimiwa Madiwani, Watendaji wa Halmashauri na Wananchi kwa ujumla.

Mkuu wa Wilaya alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwezesha mkutano huo. Aidha, alitoa shukrani zake kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumuamini na kumteua kuwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro.

Alieleza kuwa alipata taarifa kuwa upo mpango wa Manispaa ya Morogoro kuwa Jiji hivyo aliahidi atashirikiana na Waheshimiwa Madiwani na Wataalam kufanikisha adhma hiyo. Pia alieleza kuwa ili kuweza kufikia moja ya vigezo vya Halmashauri ya Manispaa kuwa Jiji ni kuongeza mapato hivyo aliahidi kufanya yafuatayo:-

i.Ataunda vikosi kazi vya kusimamia ukusanyaji mapato na ataziba mianya ya upotevu wa mapato ya Halmashauri..
ii. Atawasimamia Wataalamu wa Halmashauri kukamilisha ujenzi wa miradi ya maendeleo.
iii. Aliwaomba Waheshimiwa Madiwani wawaamini Wataalamu wa Manispaa na kuwapa ushirikiano ili uweza kufikia malengo ya Manispaa ya Morogoro kuwa Jiji.

Aidha, Mstahiki Meya aliwatambulisha viongozi walioalikwa kuhudhuria mkutano huo.

**HMM/BM/45/ 2022/2023 Kuridhia agenda za mkutano**

Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo:-

1. Kufungua Mkutano
2. Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.
3. Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 25/10/2022 (taarifa za Kata) na tarehe 27/10/2022 (kawaida)
4. Yatokanayo na mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 27/10/2022.
5. Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo:-
   5.1 Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.
   5.2 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.
   5.3 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.
   5.4 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.

5.5 Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Waheshimiwa Madiwani kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023

6. Taarifa ya mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani na Wataalam kuhusu kufanya vikao na mikutano kwa kutumia mifumo ya kidigitali yaliyofanyika tarehe 16 – 20/12/2022.
7. Kufunga Mkutano.

HMM/BM/46/2022/2023 Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.

**1.0 Kuhusu upungufu wa Madawati katika Shule ya Sekondari Kingalu Kata ya Kilakala:-**

Mjumbe alieleza kuwa Shule ya Sekondari Kingalu Kata ya Kilakala ina upungufu mkubwa wa madawati hali iliyosababisha wanafunzi zaidi ya 100 kukaa chini. Mjumbe alitaka kujua Halmashauri ina mpango gani wa kutatua changamoto hiyo.

**Majibu**

Mkurugenzi wa Manispaa alipokea taarifa hiyo na aliahidi atafuatilia na kufanyia kazi haraka ndani ya wiki mbili. Aidha, alieleza kuwa ili kutatua kero hiyo kwenye shule nyingine Halmashauri itatenga fedha kwenye bajeti ya Halmashauri ya mwaka wa fedha 2023/2024.

**2.0 Kuhusu Kata ya Sultan Area kuwa na Shule yake ya Sekondari:-**

Mjumbe aliuliza ni lini Halmashauri itajenga Shule ya Sekondari ya Kata ya Sultan Area..

**Majibu**

Mkurugenzi wa Manispaa alianza kwa kumshukuru Mheshimiwa Diwani wa Kata kwa kupambania Wananchi wa Kata yake. Kuhusu ombi la kujenga Shule ya Sekondari ya Kata alieleza kuwa Kata haina eneo la kujenga Shule ya Sekondari lakini aliahidi ndani ya siku 3 Kata itakabidhiwa eneo na hati miliki ya kujenga Shule ya Sekondari Kiegea 'A'

**3.0 Kuhusu kudhibiti mafuriko Kata ya Lukobe, Kihonda na Mkundi :-**

Mjumbe alitaka kujua Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya barabara na kufukua mitaro ili kudhibiti mafuriko kwenye Kata ya Lukobe, Kihonda na Mkundi.

**Majibu**

Ilielezwa kuwa kufuatia mafuriko yaliyotokea katika maeneo ya Kata za Lukobe, Kihonda na Mkundi tarehe 13/01/2023 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya zilitoa misaada ya kibinadamu kwa Wananchi walioathirika na mafuriko hayo ikiwemo kuwapa vyakula, hifadhi ya malazi na elimu waache kujenga maeneo ya mabondeni na kwenye mikondo ya maji.

Aidha, taarifa ya uharibifu wa mali na miundombinu iliandaliwa na kupelekwa Kamati ya Maafa ya Mkoa kuomba msaada zaidi.

**4.0 Kuhusu ubovu wa miundombinu kwenye Kata ya Mindu:-**

Mjumbe alieleza kuwa Kata ya Mindu, miundombinu ya barabara kuelekea Zahanati ya Mgaza na Zahanati ya Lugala ni mibovu, Mjumbe aliuliza Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina mpango gani wa dharura kuitengeneza ili kuzuia mafuriko hasa kwa msimu wa mvua.

**Majibu**

Mkurugenzi wa Manispaa alimpongeza Mheshimiwa Diwani kwa kuwapelekea maendeleo Wananchi wake. Aidha, Mkurugenzi wa Manispaa alikiri kuwepo kwa ubovu wa miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro. Alifafanua kuwa miundombinu ya barabara inasimamiwa na TARURA Wilaya, hata hivyo Manispaa ya Morogoro imetenga kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 kiasi cha **Tshs. 400,000,000.00** kununua greda na imeruhusiwa na Serikali na litatumika kuchonga barabara za Manispaa kwa usimamizi wa TARURA.

**5.0 Kuhusu umaliziaji wa Zahanati na upelekaji wa vifaa tiba kwenye Zahanati na Vituo vya Afya ili viweze kuhudumia wagonjwa kwa asilimia 100:-**

Mjumbe aliuliza ni lini Halmashauri itamalizia ujenzi wa Zahanati na itapeleka vifaa tiba kwenye Zahanati na Vituo vya Afya vilivyojengwa na Manispaa ili viweze kuhudumia wagonjwa kwa asilimia 100. Aidha, Mjumbe alimpongeza Mhe. Abdulaziz Mohamed Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini kwa kusaidia kutoa vifaa tiba kwenye baadhi ya Zahanati na vituo vya Afya vya Manispaa**.**

**Majibu**
Ilielezwa kuwa Halmashauri inamalizia zahanati na Vituo vya Afya zilizoanza kujengwa na Wananchi. Aidha, majengo yakikamilika Serikali inazisajili na kuleta Wafanyakazi pamoja na vifaa tiba ili kuanza kutoa huduma.

**6.0 Kuhusu ombi la kujenga wodi ya kupumzikia akina mama wazazi na watoto katika Kituo cha Afya Sabasaba:-**

Mjumbe alieleza kuwa katika Kituo cha Afya Sabasaba kumejengwa chumba cha upasuaji cha wazazi na watoto. Mjumbe alitaka kujua ni lini Halmashauri itajenga wodi ya kupumzika baada ya upasuaji kabla ya kuruhusiwa.

**Majibu**
Mkurugenzi wa Manispaa alieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Halmashauri itajenga vyumba vya upasuaji (Theatre) na wodi za kupumzikia wagonjwa kwenye Vituo vya Afya vya Sabasaba na Mafiga ili kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro.

**7.0 Kuhusu upungufu wa vyumba 15 vya madarasa shule ya msingi Mafiga 'B' na Mafiga 'A' pamoja na upungufu wa madawati:-**

Mjumbe alitaka kujua Halmashauri ina mpango gani wa kutatua changamoto ya upungufu wa vyumba 15 vya madarasa katika shule ya msingi Mafiga 'B' na upungufu wa madawati shule ya msingi Mafiga 'A' hali inayosababisha wanafunzi 200 kukaa chini.

**Majibu**
Ilielezwa kuwa Halmashauri ina mkakati wa kuhakikisha katika mwaka wa fedha 2023/2024 inatenga fedha **Tshs. 500,000,000.00** za kutengeneza madawati **6000** ili kuondoa kero ya wanafunzi kukaa chini. Aidha, Halmashauri imejiwekea mkakati wa kukamilisha maboma **48** ya vyumba vya madarasa hivyo kumaliza kabisa tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa katika mwaka wa fedha 2023/2024.

| | |
|---|---|
| HMM/BM/47/2022/2023 Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 25/10/2022 (Taarifa za Kata) na tarehe 27/10/2022 (Kawaida) | Mihtasari haikuwa na masahihisho hivyo ilithibitishwa kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi za mikutano. |
| HMM/BM/48/2022/2023 Yatokanayo na mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 27/10/2022. | **1.0 Kuhusu mikataba ya kuwapangisha Wafanyabiashara katika Stendi ya Daladala Mafiga.**<br>**Azimio**<br>Baraza la Madiwani lilitoa muda wa siku saba (wiki moja) kuanzia tarehe 28/10/2022 Wafanyabiashara wa stendi ya Daladala Mafiga wasaini mikataba ya kupangishwa maeneo kwa mita moja ya mraba **Tshs. 500.00** na waanze kulipa.<br><br>**Utekelezaji**<br>Agizo limezingatiwa. Menejimenti ilifanya mawasiliano na Mbia (SUA) kupata maoni yao juu ya kupangisha eneo hilo kwa kiwango cha **Tshs. 500.00** kwa mita moja ya mraba. Pia (SUA) imeridhia na kukubaliana na maoni ya Baraza ya kuwasainisha mikataba ya wapangaji. Mikataba imeandaliwa na tayari wafanyabiashara wameanza kuchukua mikataba yao.<br><br>**Mjadala**<br>Mjumbe alitaka kujua ni kwa nini magari hayaingii stendi ya Daladala Mafiga kama Baraza lilivyoagiza.<br><br>**Ufafanuzi**<br>Ilielezwa kuwa suala hilo kiutendaji ni la Wadau mbalimbali ambao wapo chini ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Wadau hao ni LATRA, Polisi, na Wadau wa vyombo vya usafirishaji abiria hivyo linaendelea kufanyiwa kazi. |

HMM/BM/49/2022/2023 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo.

**1.0 Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.**

Taarifa iliwasilishwa, iliungwa mkono, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**Mjadala**

Wajumbe waliipongeza Kamati ya Fedha na Uongozi pamoja na Menejimenti kwa kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2023 kwa vyanzo vya ndani kwa kukusanya **Tshs. 3,410,812,250.08** kati ya lengo la kukusanya **Tshs. 3,163,600,000.00** sawa na asilimia **107.81.**

Mjumbe alitaka kujua ni kiasi gani cha fedha zilizokusanywa **Tshs. 3,410,812,250.00** sawa na asilimia **60** kilipelekwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa zipo bakaa za **Tshs. 450,000,000.00** ambazo zitatumika kwenye robo ya tatu Januari – Machi, 2023 kumalizia maboma ya shule za msingi na zahanati na mapato ya salio la robo ya tatu yatatumika katika robo ya nne Aprili – Juni, 2023.

**Kuhusu viosk vya SIDO:-**

Mjumbe alitaka kujua mazungumzo ya Menejimenti na Wafanyabiashara wa viosk vya SIDO ya kulipa kodi ya pango ya **Tshs. 50,000.00** kwa kiosk kwa mwezi yamefikia hatua gani.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa wafanyabiashara wote wametambuliwa na wameshaanza kulipa kodi ya pango ya **Tshs. 50,000.00** kwa mwezi.

Baada ya mjadala Wajumbe waliridhia taarifa.

**2.0 Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.**

Taarifa iliwasilishwa, iliungwa mkono, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**Mjadala na maagizo**
**Kuhusu changamoto kwa baadhi ya vikundi/wazabuni kushindwa kuzoa taka kwenye Mitaa**
Ilielezwa kuwa Kata ya Mbuyuni na Mazimbu vikundi kazi havina mashine za POS hivyo vikundi vinakusanya mapato kiholela bila kutoa risiti za EFD Mjumbe alitaka kujua mapato wanayokusanya yanakwenda wapi.

**Ufafanuzi**
Ufafanuzi ulitolewa kuwa hilo ni kosa kikundi/Mzabuni kukusanya mapato bila kutoa risiti ya EFD hivyo Mkurugenzi wa Manispaa aliwaagiza Watendaji wa Kata wote wahakikishe kuwa wanawasimamia Wananchi wanapolipa fedha zao wanapewa risiti za EFD.

Aidha, aliahidi kulifanyia kazi haraka tatizo la vikundi vya usafi wa mazingira vya Kata za Mbuyuni na Mazimbu kutokuwa na mashine za POS sanjari na Kata zingine.

Mjumbe alieleza kuwa Menejimenti inatakiwa ijiridhishe kuwa vikundi vyote vinakuwa na POS mashine. Aidha, ilielezwa kuwa POS mashine ambazo awali walipewa vikundi kisha zilichukuliwa na Menejimenti kufanyiwa matengenezo zirudishwe kwenye vikundi.

**Agizo**
Wajumbe waliagiza kuwa Menejimenti iwasilishe taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi ikionesha ni miezi mingapi vikundi vya usafi wa mazingira vimekusanya ushuru wa kuzoa taka taka bila POS mashine na kiasi kilichokusanywa kwenye Kata zote na ielezwe fedha ziko wapi.

**3.0 Taarifa ya Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.**
Taarifa iliwasilishwa, iliungwa mkono na Wajumbe waliipokea.

**Mjadala**
**Kuhusu Wananchi wanaogonga kokoto Kata ya Kilakala**
Baraza lilishauri kuwa wanaogonga kokoto Kata ya Kilakala waelimishwe waache kazi hiyo kwani wanaharibu mazingira badala yake washauriwe kufanya biashara nyingine.

Wajumbe waliridhia taarifa hiyo.

| | |
|---|---|
| | **4.0 Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.**<br>Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa, iliungwa mkono na Wajumbe waliiridhia.<br><br>**5.0 Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023.**<br>Mwenyekiti aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Maadili ya Waheshimiwa Madiwani kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Desemba, 2022/2023. Aidha, ilielezwa kuwa katika kipindi hicho kulikuwa na tuhuma za ukiukwaji wa Kanuni za Maadili za Madiwani za mwaka 2000 ambazo zilimuhusu Mjumbe mmoja. Baada ya Wajumbe kujadili kama Kamati ya Halmashauri nzima iliamua kumsamehe. |
| HMM/BM/50/ 2022/2023 Taarifa ya mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani na Wataalamu kuhusu kufanya vikao na mikutano kwa kutumia mifumo ya kidigitali yaliyofanyika tarehe 16-20/12/2022. | Taarifa ya mafunzo iliwasilishwa na Wajumbe waliipokea na kuiridhia. |
| HMM/BM/51/ 2022/2023 Kufunga Mkutano | Kabla ya kufunga mkutano, Mstahiki Meya alimkaribisha Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini ili aweze kuongea machache.<br><br>Mwenyekiti wa Chama alisema Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro liliamua ugongaji wa kokoto kwenye mto Morogoro usitishwe kwa kuwa unaharibu mazingira. Aidha, Baraza liliamua kuwatafutia eneo la nyama choma Lugono ambapo Halmashauri iliwawekea miundombinu ya choo hivyo alishauri Wananchi wanaotaka kufanya shughuli hizo waende huko. |

**Kuhusu Kituo cha Afya Mafiga kupelekewa Jenereta.**
Alishauri kuwa Kituo cha Afya Mafiga kipelekewe Jenereta kubwa ili kusaidia wakati umeme wa TANESCO unapokatika.

Mstahiki Meya aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani na Wataalamu kwa kumaliza vikao vya robo ya pili 2022/2023. Alieleza kuwa vikao vinavyofuata ni vya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 hivyo aliwasihi kila mtu kwa nafasi yake abuni na kupendekeza chanzo kipya cha mapato ili Halmashauri iweze kuongeza mapato yake.

Baada ya kusema hayo Mstahiki Meya alifunga Mkutano saa 8:20 mchana.

Muhtasari umethibitishwa tarehe ………………………………………………………

| | |
|---|---|
| ……………………………… | ……………………………… |
| Mhe. Pascal M. Kihanga | Ndg. Ally H. Machela |
| MSTAHIKI MEYA | MKURUGENZI WA MANISPAA |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 08/02/2023**

| MUHT. NA | AZIMIO | MTEKELEZAJI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| HMM/BM/45/2022/2023 Taarifa ya Kamati za Kudumu na Kamati nyinginezo | **2.0 Kuhusu changamoto kwa baadhi ya Vikundi/ Wazabuni kushindwa kuzoa taka kwenye Mitaa.** Wajumbe waliagiza kuwa Menejimenti iwasilishe taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi ikionesha ni miezi mingapi vikundi vya usafi wa Mazingira vimekusanya ushuru wa kuzoa taka bila mashine ya POS na kiasi kilichokusanywa kwenye Kata zote na ielezwe fedha zipo wapi. | Mkuu wa Kitengo cha Usafishaji na Udhibiti wa Taka<br><br>Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu wa Manispaa | Agizo limezingatiwa. Mashine hizo zilichukuliwa tarehe 14/08/2022 na kurejeshwa tarehe 10/02/2023 kwa kuwa hairuhusiwi kukusanya mapato bila POS. Timu imeundwa na Mkurugenzi kufuatilia suala hilo ingawa kwa sasa wanatumia POS. |